

Mauzo nyama nje yazidi kuongezeka

Na John Mhala, Arusha

WIZARA ya Mifugo na Uvuvu imesema ndani ya miezi sita mwaka huu Tanzania imeuza nyama tani 10,000 katika nchi za Bara la Asia na kuvunja rekodi ya mwaka jana.

Akifungua warsha ya siku saba ya wataalamu wa sekta ya mifugo kutoka nchi za Kusini mwa Afrika, Waziri wa wiz... hiyo, Mashimba Ndaki alisema ongezeko la mauzo ya nyama nje ya nchi ni matokeo ya ziara za Rais Samia Suluhu Hassan ughaibuni kuvuta wawekezaji.

Alisema hadi Desemba mwaka huu huenda Tanzania ikaiza nyama nyingi zaidi kuliko miaka yote kwa kuwa mwaka jana iliuzza nyama tani 7,000 tu.

Ndaki alisema wizara hiyo imeweka mpango kazi wa kuhakikisha wafugaji wanafuga mifugo bora ili kumpatia mlaji bidhaa bora kwa maslahi ya nchi.

Alisema wizara hiyo imepanga kuboresha sekta ya mifugo kwa kufuga kisasa katika vituo vya ng'ombe na mbuzi ili kuwe na mifugo bora kumudu ushindani sokoni kimataifa kwa maslahi ya nchi.

Alisema serikali imepanga kushirikiana na nchi wanachama wa Jamhuri ya Uchumi Kusini mwa Afrika (SADEC) kuboresha mifugo na kuwa na nyama bora kwa ajili ya kuuzwa nje ya nchi.

Uhifadhi bahari unavyochangia uchumi wa buluu

Na Rahma Suleiman,
ZANZIBAR

MKURUGENZI wa Idara ya Uhifadhi wa Bahari, Dk Makame Omar Makame amesema uhifadhi wa bahari ndiyo msingi mkuu wa uchumi wa buluu katika kuleta maendeleo nichini kupitia sekta ya uvuvi, utalii na ufgaji wa mazao ya bahari.

Aliysema hayo Mjini Zanzibar, katika mukutano wa mrejesho kwâ wadau wa serikali na wa utalii kuhusu uanzishwaji na utekelezaji wa kazi za uhifadhi wa bahari.

Dk. Makame aliwataka wadau mbalimbali kusimamia uhifadhi wa bahari kutokana na mnyororo mzima wa thamani wa utalii uhatokana na mazingira mazuri ya bahari na rasilimali zake.

"Ikiwa tutaathiri maeneo ya hifadhi kutapelekea kuporomoka kwa ajira za vijana kupitia utalii nichini jambio ambalo ni kichochezi cha kuanguka kwa uchumi nichini," alisema.

Dk. Makame alisema Idara iyo katika harakati ya kuweka matumbawé bandia kwa ajili ya kurejesha viumbi vilivyoadimika baharini ili kuungeza vivulio na thamani ya utalii.

Naye Ofisa Mkuu wa Uhifadhi kutoka Idara ya Uhifadhi wa Bahari, Mohammed Choum, aliwataka wadau mbalimbali na vyombo vya ulimzi na usalama kuwa na ushirikiano wa pamoja katika hifadhi shirikishi na kufanya doria za mara kwa ili kudhibiti uvuvi haramu.

Aliwataka wavuvi kuwa mstari wa mbele kusimamia maeneo ya hifadhi katika kuwadhibiti waharibifu wa rasilimali za bahari kwa ajili ya kujilinda uchumi wa buluu.

Kwa upande wao watendeza watatu walimba Idara ya uhifadhi wa bahari kuwekeea kamati msaalumu ya usafi na utunzaji we mazingira kutokana na uharibifu mikubwa unaotendeka katika hifadhi

**Na R
ZAN**

**V
Haro
ka w.
Katib
kupa**

**Ak
wa h
cha
Msaa
kuna
jamili
masi
rathu,
na i
migo**

**Ali
tizo l
idara
wao v**